



POLISI WA KENYA

MKATABA WA HUDUMA

MAONO:

Matarajio yetu ni kutoa huduma kuambatana na viwango bora vya kimataifa tukizingatia usikivu na utaalamu wa kazi.

LENGO:

Kutoa huduma zetu kwa njia inayoridhisha matarajio ya wateja wetu kwa kuzingatia kanuni za sheria zetu na utangamano baina yetu na wanainchi ili kuleta mazingira mazuri ya kijamii, uchumi na maendeleo ya kisiasa katika nchi yetu.

MAADILI YA MSINGI:

- Umakini na usikivu katika utekelezaji wa majukumu yetu.
- Uadilifu na heshima wakati wote;
- Ushirikiano na washikadau wote;
- Undugu na uhusiano mwema kati ya maafisa;
- Haki na kutii sheria nyakati zote;
- Nidhamu na utaalamu umedumishwa katika kikosi cha polisi kwa mujibu wa sheria;
- Kuhakikisha maarisa wameajiriwa kwa kuzingatia hali ya jinsia na bila ubaguzi;
- Kuhamasisha, kulinda na kuheshimu haki za kimsigni za wateja wetu.

MAJUKUMU YETU:

- Kutoa usaidizi kwa uma unapohitajika;
- Kudumisha utiifu wa sheria na utangamano;
- Kuhifadhi amani;
- Kulinda maisha na mali;
- Kuchunguza visa vya uhalifu;
- Kuendeleza upelelezi ili kupata habari kuhusu uhalifu kwa wakati uliofaa;
- Kuzuia na Kuvumbua visa vya uhalifu;
- Kutia nguvuni waliovunja sheria;
- Utekelezaji wa sheria na kanuni zilizomo;
- Kutekeleza wajibu wowote ule kulingana na amri ya Inspekta Generali wa Polisi kwa mujibu wa sheria za nchi.

HUDUMA ZETU

HUDUMA	MAJUKUMU YA MTEJA	MALIPO	MUDA
Kutoa usaidizi kwa uma unapohitajika	Kuzungumza na afisa yeyote wa Polisi	Hakuna malipo	Hapo kwa Hapo
Kudumisha utiifu wa sheria na utangamano;	Ushirikiano	Hakuna malipo	Kwa muda usiozidi masaa ishirini na manne
Kuhifadhi amani;	Ushirikiano	Hakuna malipo	Kwa muda usiozidi masaa ishirini na manne
Kulinda maisha na mali;	Ushirikiano	Hakuna malipo	Kwa muda usiozidi masaa ishirini na manne
Uchunguzi wa visa vya uhalifu	Ukweli na usahihi wa kisa na wahusika katika ripoti	Hakuna malipo	Kwa muda wa siku saba
Kuendeleza upelelezi ili kupata habari kuhusu uhalifu kwa wakati uliofaa;	Ushirikiano	Hakuna malipo	Kwa muda usiozidi masaa ishirini na manne
Kuzuia na Kugundua visa vya uhalifu;	Ushirikiano	Hakuna malipo	Kwa muda usiozidi masaa ishirini na manne
Kutia nguvuni waliovunja sheria;	Ushirikiano	Hakuna malipo	Hapo kwa Hapo
Kutekeleza sheria na kanuni zilizomo;	Ushirikiano	Hakuna malipo	Kwa muda usiozidi masaa ishirini na manne
Kutekeleza wajibu wowote kutoka kwa Inspekta Generali wa Polisi kwa mujibu wa sheria.	Ushirikiano	Hakuna malipo	Kwa muda usiozidi masaa ishirini na manne
Kutembelea na kushughulikia eneo la uhalifu;	Kutoingilia eneo la uhalifu ili kuhifadhi ushahidi	Hakuna malipo	Kwa muda usiozidi masaa mawili
Kutoa huduma za kusindikiza kwa wanaohitaji huduma hii;	Arifa ya mapema na notisi la ombi katika masaa ishirini na manne	<i>Kwa maelezo zaidi rejea katika Gazeti la Kenya toleo la tarehe 12 Noveba, 2004</i>	Dakika kumi
Kukabiliana na uhalifu au dhiki katika hali ya dharura;	Ripoti kamili kuhusu kisa na mahali kilipotokea	Hakuna malipo	Hapo kwa Hapo
Utoaji wa fomu ya P3 na hati nyingine za Polisi kama;	Habari za kweli na sahihi	Hakuna malipo Hakuna malipo Hakuna malipo Hakuna malipo	Dakika kumi na tano

(fomu hizi pia zinaweza kupatikana katika tuvuti, anwani: www.kenyapolice.go.ke)			
Kuwasilisha kortini washukiwa waliozuiliwa katika kituo cha polisi.	Ushirikiano na kuwa tayari kutoa ushahidi dhidi ya mshukiwa mbele ya koti punde inapohitajika kufanya hivyo	Hakuna malipo	Kwa muda usiozidi masaa ishirini na manne au siku ya korti inayofuata
Katatua matukio ya msongamano wa trafiki	Kutilia mkazo kwa kufuata kanuni za barabara	Hakuna malipo	Dakika kumi na tano
<p>TUNAJITOLEA</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kuwa mtekelezi na mdamkivu katika utoaji wa huduma; • Kuwa na uadilifu na heshima wakati wote; • Kudumisha ushirikiano na washikadau wote; • Kudumisha undugu na uhusiano mwema kati ya maafisa; • Kutenda haki na kutii sheria katika shughuli zetu zote; • Kuhakikisha nidhamu na utaalumu umedumishwa katika kikosi cha Polisi; • Kuhakikisha maafisa wameajiriwa kwa kuzingatia hali ya jinsiana bila mapendeleo; • Kuhamasisha, kulinda na kuheshimu haki za kibinadamu za wateja wetu. 			
<p>MALALAMIKO DHIDI YA POLISI</p> <p>Mtu yeyote ambaye hajaridhishwa na huduma zetu anaweza kuwasilisha malalamishi kwa afisa mku wa kituo cha polisi (OCS). Kama hataridhika na usaidizi wa OCS, ako huru kuwasilisha malalamishi yake kwa mkuu wa Polisi anayesimamia wilaya (OCPD), au kwa Kamanda wa Kaunti, Idara ya maswala ya ndani au kwa Naibu wa Inspekta Generali wa Polisi katika makao makuu ya Polisi (VIGILANCE HOUSE) kulingana na kesi.</p> <p>MAELEZO ZAIDI</p> <p>Kwa maelezo zaidi unaweza kuwasiliana na makao makuu ya Polisi. Simu: +254(020-3341411) au Idara inayoshughulikia malalamishi - simu: + 254 (020) -2221969. Wakati wa dharula piga nambari 999 ama 112 ambayo hailipishwi.</p>			

KAULIMBIU: UTUMISHI KWA WOTE TOLEO JIPYA 2014.